



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

TANGAZO

Utangulizi

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inutangazia umma kuwa imepokea barua kutoka Ubalizi wa Ireland kuwa unatoa ufadhili wa Masomo ya masuala ya jinsia kwa ngazi ya shahada ya uzamili Nchini Ireland. Ufadhili huo unatolewa kupitia “ **Irish Aid Fellowship Programme**” kwa Mtanzania yeyote mwenye sifa anayeishi hapa nchini.

Programu na Vyuo

Zifuatazo ni programu zinazofadhiliwa na vyuo vinavyoendesha Mafunzo:

- ‘**M.A in Women, Gender and Society**’ katika Chuo Kikuu cha Dublin: <http://bit.ly/2tlYixn>
- ‘**M.A in Gender, Globalization and Rights**’ katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Ireland, Galway: www.bit.ly/c9SC9i
- ‘**M.A. in Public Advocacy and Activism**’ katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Ireland, Galway: www.nuigalway.ie/publicadvocacy

Sifa Zinazohitajika

Mwombaji unatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

- Uwe Raia wa Tanzania;
- Uwe Mkazi wa Tanzania;
- Uwe na sifa zinazohitajika kwa ajili ya udahili wa ngazi ya Shahada ya Uzamili kwenye Taasisi za Elimu ya Juu za Ireland;
- Uwe umefanya mihani ya Lugha ya Kiingereza (IELTS) na kufaulu wa wastani ya 6.5 au zaidi wakati wa kuwasilisha maombi;
- Uoneshe dhamira ya dhati katika kuleta maendeleo ya nchi;
- Uwe unaomba kuanza kozi mwaka na usiwe ulishaanza masomo kabla ya tangazo;
- Uwe tayari kuanza masomo mwaka 2018/19 na si vinginevyo;
- Uwe umewasilisha barua ya utambulisho kutoka kwa mwajiri au kutoka kwa mtu mwingine anayemfahamu mwombaji.

Tangazo hili linapatikana pia kwenye tovuti ya Wizara: www.mcdgc.go.tz na kwa taarifa zaidi kuhusu ufadhili huu, tembelea tovuti ya ubalizi: http://www.dfa.ie/irish-embassy/Tanzania/news_and_events/latest_news/fellowship-training_programme-2018.html. Maombi yatumwe kupitia anuani ya barua pepe: TanzaniaFellowships@dfa.ie. Wanawake wanahimizwa kuomba masomo na ufadhili huu. **Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi haya ni tarehe 2 Januari, 2018**